SHERIA YA UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI
(SURA 413)

# KANUNI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA VIGEZO NA MASHARTI YA KUTOA HUDUMA ZINAZODHIBITIWA ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI


*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina
2. Matumizi
3. Tafsiri

SEHEMU YA PILI
VIWANGO VYA CHOMBO NA MAHITAJI YA USALAMA

4. Kufuata viwango
5. Marekebisho ya chombo
6. Utaratibu wa huduma na matengenezo
7. Huduma na matengenezo

SEHEMU YA TATU
VIWANGO MAALUM KWA VYOMBO VYA USAFIRI WA UMMA

8. Viwango na mahitaji ya usalama kwa vyombo vya usafiri wa umma
9. viwango na mahitaji ya usalama kwa vyombo vya kusafirisha mizigo
10. Viwango na maahitaji ya usalama kwa vyombo vinavyosafirisha bidhaa hatarishi
11. kuondoa masharti
12. Viwango na mahitaji ya usalama kwa vyombo vya huduma ya usafiri wa kukodi
13. Mahitaji ya huduma
14. Muda wa basi kusimama kituo cha njiani
15. Matakwa ya kuwa na bima
16. Mahitaji ya kuwa na wataalam

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA JUMLA

17. Matakwa ya kutoa huduma kupitia kampuni au ushirika
18. Adhabu ya jumla

19. Kumzuia Afisa wa Mamlaka
20. Notisi ya kujiondoa kutoa huduma
21. Mapitio
22. Kufutwa

---

JEDWALI

---

Tangazo la Serikali Na. ……………… la tarehe …………………

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI
(SURA. 413)

# KANUNI

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 41(1)(c))*

## KANUNI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA VIGEZO NA MASHARTI YA KUTOA HUDUMA ZINAZODHIBITIWA ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini na Vigezo na Masharti ya kutoa Huduma zinazodhibitiwa za Mwaka 2023

matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa vyombo vinavyokusudiwa kutoa huduma za usafirishaji kibiashara Tanzania Bara.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama itakapoelezwa vinginevyo-

Sura 413 — "Sheria" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

Sura 413 — "Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hiyo;

Sura 130 — "Shirika la Viwango" maana yake ni Shirika la Viwango Tanzania

"bidhaa hatarishi" maana yake ni dutu au kifaa ambacho kina hatarisha maisha, mali au mazingira kutokana na kemikali au dutu iliyo nayo;

Sura 413 — "Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 15 cha Sheria;

"leseni" maana yake ni leseni za kutoa huduma za usafirishaji kwa njia ya barabara zinazotolewa na Mamlaka kwa ajili ya huduma inayodhibitiwa;

"kelele" maana yake ni sauti zenye kadhia kwa binadamu ambazo zinaweza kusababisha madhara hasi kwa afya yake au mazingira;

"bidhaa za kukera" maana yake ni bidhaa zinazoweza kuleta karaha kama vile damu kavu, maiti, nyama ya mnyama aliyekufa, mifupa, samadi, nguo chafu ambazo uchafu wake hautokani na mafuta ya gari, mzoga, mboga zilizooza, mafuvu na viungo vingine vya binadamu;

“mtoa huduma” maana yake ni mmiliki wa leseni hai ya uendeshaji wa chombo kinachotoa huduma ya usafiri kibiashara;

Sura 297

“karakana iliyosajiliwa” maana yake ni karakana iliyokidhi viwango na kusajiliwa na Shirika la Viwango kwa ajili ya utengenezaji wa vyombo vinavyotaoa huduma za usafiri kibiashara;

"barabara" maana yake ni barabara kuu, barabara za kawaida, barabara za mitaa, daraja, kalvati, kivuko, maegesho ya magari, njia ya waenda kwa miguu au njia ya hatamu ambapo vyombo vya usafiri vinaweza kupita na umma unaweza ukafika endapo barabara hizo zimezuiwa au vinginevyo kwa masharti yoyote yale isipokuwa barabara gegedu kwenye maeneo ya makazi;

“chombo” maana yake ni chombo kinachoendeshwa kwa mitambo au umeme kilichokusudiwa kutoa huduma ya usafirishaji kibiashara;

## SEHEMU YA PILI
## VIWANGO VYA CHOMBO NA MAHITAJI YA USALAMA

Kufuata viwango

4. (1) Mtoa huduma anayeendesha chombo cha usafiri kibiashara anatakiwa kuhakikisha kuwa chombo kinakidhi vigezo vilivyowekwa mamlaka zinazohusika na masuala ya kuweka viwango.

(2) Mtoa huduma atakayekiuka masharti ya kanuni ndogo (1) atakuwa ametenda kosa.

Mahitaji ya jumla ya usalama kwa vyombo vya kibiashara

5. (1) Mtoa huduma wa chombo cha biashara anapaswa kuhakikisha kuwa-

(a) sakafu ya chombo cha usafiri isiwe ya kuteleza, kushika kutu na chombo kiwe kimetengenezwa katika hali ya kumkinga abiria dhidi ya vumbi, mvuke, mafusho, kelele, hitilafu ya umeme, dutu hatarishi, kuvuja kwa mafuta na vilainishi kulingana na viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango;
(b) milango na madirisha ya chombo kinachotoa huduma lazima ifunguke na kufunga kwa urahisi na isiruhusu vumbi au maji kuingia sehemu anapoketi abiria;
(c) usukani wa chombo uwe mbele upande wa kulia wa chombo;
(d) mwamba wa chombo, mineso, ekseli na rimu za vyombo vya usafiri kwa umma viwe vimefungwa madhubuti na havijapasuka wala kuungwa kwa umeme;
(e) chombo hakitaruhusiwa kuendeshwa, kutoa huduma au kuegeshwa barabarani au mahali pengine kama hakijafanyiwa matengenezo pamoja na vifaa vyake vyote kwa mujibu wa mahitaji ya viwango vya usalama kutoka Shirika la Viwango.
(f) chombo kisiwe kimeungwa minyororo, vyuma, vifaa, gurudumu au vifaa vingine ndani au nje ya chombo na kuhatarisha maisha ya abiria na watu wengine;
(g) chombo kinakidhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango kwa ajili ya vyombo vinavyobeba mizigo

(2) Mtoa huduma atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia atalipa faini isiyopungua Shilingi laki mbili na isiyozidi Shilingi laki tano au kifungo kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi miezi mitatu jela au vyote.

mabadiliko ya chombo

6. (1) Mtoa huduma wa vyombo vinavyotoa huduma ya usafiri kibiashara anaweza kubadilisha chombo chake isipokuwa mabadiliko hayo yanapaswa kufanyika-
   a) Kwa kuzingatia vigezo vilivyoainisha na mtengenezaji na kuidhinishwa na shirika la viwango; au
   b) Katika karakana iliyothibitishwa na Shirika la Viwango.

(2) Pasipokuathiri masharti yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), basi halitaruhusiwa kuundwa kwenye mwamba ya lori.

Huduma na matengenezo

7. (1) Pamoja na ratiba ya kawaida ya matengenezo ya chombo, mtoa huduma wa chombo cha biashara anapaswa kuahakikisha kwamba-
   a) Chombo cha biashara kinafanyiwa matengenezo ya mara kwa mara katika karakana iliyosajiliwa angalau kwa kiwango cha chini kwa mujibu wa mwongozo wa mtengenezaji; na
   b) msimamizi au mwendeshaji wa karakana iliyosajiliwa-
      (i) anakuwa na angalau stashahada ya ufundi wa mitambo au magari; na
      (ii) anatoa kadi ya kumbukumbu ya matengenezo yaliyofanyika kwa kila chombo kilichotengenezwa.

(2) Mtoa huduma wa chombo cha biashara anapaswa kuhakikisha anaweka kadi ya kumbukumbu ya matengenezo yaliyofanyika kwenye chombo.

## SEHEMU YA TATU
## VIWANGO MAALUM NA MAHITAJI YA USALAMA

Viwango na mahitaji ya usalama kwa vyombo vya usafiri wa umma

8. Mtoa huduma wa chombo cha usafiri wa umma anapaswa kuhakikisha kuwa -
   a) chombo kinakuwa na nafasi kwa ajili ya kuhudumia abiria wenye mahitaji maalum;
   b) abiria hawakai ndani ya chombo wakati chombo kikifanyiwa matengenezo au kujazwa mafuta; na
   c) chombo cha usafiri wa umma hakibebi wanyama hai, bidhaa hatarishi au zinazokera;

viwango na mahitaji ya usalama kwa vyombo vya kusafirisha mizigo

9. Mtoa huduma wa chombo cha kusafirisha mizigo anapaswa kuhakikisha kuwa-
   a) chombo cha kusafirisha mizigo kiwe kimetenganisha sehemu ya dereva na sehemu ya mizigo ili kuzuia mwingiliano baina ya mizigo na dereva; na
   b) mizigo iliyobebwa iweze imefunikwa ili kuzuia kudondosha kwa chembechembe, vumbi, unyevu, kuvuja au moshi.

Viwango na maahitaji ya usalama kwa vyombo vinavyosafirisha bidhaa hatarishi

10. Mtoa huduma wa chombo cha kusafirisha bidhaa hatarishi anapaswa kuhakikisha kuwa -
   a) chombo cha kusafirisha bidhaa hatarishi kimewekwa alama za tahadhari kwa mujibu wa viwango vilivyopitishwa katika tasnia husika;
   b) chombo cha kusafirisha bidhaa hatarishi kiwe kimetenganisha sehemu ya dereva na sehemu ya mizigo ili kuzuia mwingiliano baina ya bidhaa hatarishi na dereva;

c) bidhaa hatarishi inatakiwa kufunikwa ili kuzuia kudondoka kwa chembechembe, vumbi, unyevu, kusambaa kwa moshi au kuvuja.

kuondoa masharti

11. Bila kujali masharti ya kanuni 8, 9, au 10 Mamlaka inaweza kuondoa sharti lolote chini ya Kanuni hizi.

Viwango na mahitaji ya usalama kwa vyombo vya huduma ya usafiri wa kukodi

12. Mtoa huduma wa chombo cha usafiri wa kukodi anapaswa kuhakikisha kwamba -

(a) chombo kinakuwa na nafasi kwa ajili ya kuhudumia abiria wenye mahitaji maalum;
(b) abiria hawakai ndani ya chombo wakati chombo kikifanyiwa matengenezo au kujazwa mafuta;
(c) Pikipiki za kukodi zinapaswa kuwa na injini zenye mapigo manne; na
(d) chombo cha usafiri wa kukodi hakibebi wanyama hai, bidhaa hatarishi au zinazokera;

(2) Mamlaka inaweza kuondoa sharti lolote chini ya kanuni hii.

(3) Mtoa huduma atakayekiuka masharti ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa na atakapokutwa na hatia-

a) ikiwa ni pikipiki ya magurudumu mawili au matatu, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu thelathini lakini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo cha muda usiozidi miezi mitatu jela au vyote;
b) ikiwa ni teksi ya kukodi, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu thelathini lakini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo cha muda usiozidi miezi mitatu jela au vyote;
c) ikiwa ni mtoa huduma wa teksi mtandao, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini lakini isiyozidi shilingi elfu laki moja au kifungo cha muda usiozidi miezi mitatu jela au vyote;
d) ikiwa ni mtoa huduma wa teksi mtandao wa kushirikiana, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano lakini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo cha muda usiozidi miezi mitatu jela au vyote; na

## SEHEMU YA NNE
## VIWANGO VYA UBORA WA HUDUMA

Mahitaji ya huduma
TS. Na. 76 ya mwaka 2020
TS. Na. 77 ya mwaka 2020
TS. Na. 78 ya mwaka 2020

13. Mtoa huduma atahakikisha kuwa chombo cha huduma ya biashara kinakidhi mahitaji yaliyoainishwa chini ya Kanuni za leseni za Usafirishaji za Vyombo vya Huduma za Usafiri wa Umma, 2020, Kanuni za leseni za Usafirishaji za Vyombo vya Huduma za Usafirishaji wa Mizigo, 2020 na Kanuni za leseni za Usafirishaji za Vyombo vya Huduma za Usafiri wa Kukodi, 2020.

Muda wa basi kusimama kituo cha njiani

14. Mtoa huduma atahakikisha chombo cha biashara hakisimami kituo cha njiani kwa zaidi ya muda wa dakika tatu.

Matakwa ya kuwa na bima

15. (1) Mtoa huduma wa chombo cha huduma za biashara atahakikisha kuwa chombo chake kina kinga ya angalau bima ndogo kulingana na sheria nyingine zinazohusika.

(2) Wakati wa ajali, Mtoa huduma atawajibika kusaidia majeruhi pamoja na mali zao, mizigo na kuhakikisha wanapata haki zao kupitia bima kwa kuwasilisha taarifa ya ajali mapema na kutoa nyaraka na taarifa muhimu zinatohitajika na shirika la bima, Jeshi la Polisi na mtu mwingine yeyote anayezihitaji.

Mahitaji ya kuwa na wataalam

16. (1) Mtoa huduma anayemiliki vyombo vya usafiri visivyozidi sita anawajibika kuwa na angalau mtaalam mmoja mwenye stashahada ya masuala ya usimamizi wa logistiki na uchukuzi kutoka katika Chuo kinachotambulika.

(2) Mtoa huduma anayemiliki idadi ya vyombo vya usafiri sita au Zaidi anawajibika kuwa na angalau mtaalam mmoja mwenye stashahada ya masuala ya usimamizi wa logistiki na uchukuzi na mwajiriwa wa kudumu mwenye stashahada ya ufundi wa magari kutoka katika Chuo kinachotambulika.

(3) bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo cha (1) na (2), mtoa huduma anapaswa kuajiri dereva aliyethibitishwa na mhudumu aliyesajiliwa na Mamlaka.

Matakwa ya kutoa huduma kupitia kampuni au ushirika

17. Mtoa huduma za usafiri anayehitaji kutoa huduma kwenye njia zenye umbali wa zaidi ya kilomita mia sita anapaswa-

a) kumiliki vyombo vya usafiri visivyopungua vinne; na

b) kutoa huduma kupitia kampuni au ushirika.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA UJUMLA

Adhabu ya jumla

18. Mtu atakayepatikana na hatia kwa kosa chini ya Kanuni hizi anatawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kwa muda usiopungua miezi mitatu jela na usiozidi mwaka mmoja jela au vyote.

Kumzuia Afisa wa Mamlaka

19. Mtu anayezuia Afisa wa Mamlaka au Afisa wa Polisi katika kutekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi, ametenda kosa.

notisi ya kujiondoa kutoa huduma

20. Mtoa huduma anayekusudia kuacha kutoa huduma za usafiriji kibiashara atatakiwa kutoa notisi kwa Mamlaka kwa maandishi mwezi mmoja kabla ya kujiondoa.

Mapitio TS. Na. 73 la 2020

21. Mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Mamlaka atatakiwa kuwasilisha maombi ya

mapitio kwa maandishi kwa mujibu wa Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini za Utaratibu wa Mapitio, 2020.

Kufutwa TS. Na. 412 la 2014

22. (1) Kanuni za Vigezo na Masharti ya Kutoa Huduma Zinazodhibitiwa za SUMATRA, 2014 zinafutwa.

(2) Bila kuathiri kufutwa kwa Kanuni, leseni, miongozo au maelekezo yaliyotolewa chini au sambamba na Kanuni zilizofutwa yaliyokuwa yanatekelezwa kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, yataendelea kutumika mpaka leseni, miongozo au maelekezo yatakapo badilishwa au kufutwa na Amri, miongozo au maelekezo yatakayotolewa chini ya Kanuni hizi.

Dodoma,
………..……….., 2023

…..…………………………….
*Mwenyekiti wa Bodi*